JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI


- **NAMBA ZA SIMU**

**Mkuu wa Shule 0752610950**

**Makamu Mkuu wa Shule**

**0759013555/0789528064**

**Patron 0767886851/0620334517**

SHULE YA SEKONDARI BOGWE

S.L.P100


11/06/2023

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**

**..................................................**

**S.L.P ...........................................**

**..................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BOGWE HALMASHAURI YA MJI WA KASULU MKOA WA KIGOMA MWAKA 2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya …………… **Shule ya Sekondari Bogwe** ipo umbali wa mita 200 kutoka kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani,kaskazini mwa kituo hicho wala huitaji usafiri wa aina yeyote kutoka kituo cha mabasi hicho kuja shuleni hapa
   Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023**



## 1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 1.1 Sare za Shule

i. Suruali mbili rangi ya dark blue zenye malinda na zisiwe za kubana
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu yenye ukosi (kola)
iii. Track suit, bukta, jezi moja vyote viwe dark blue kwa ajili ya michezo
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta rangi ya dark blue
viii. Suruali mbili **(2)** rangi ya light blue yenye linda mbili na zisiwe za kubana( sare ya bweni)
ix. Tisheti (T-shirt) 2 rangi ya dark bluu Zenye fito nyeupe mikononi na shingoni

### 1.2_Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari na vitabu vya kutosha kulingana na tahasusi yake
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Godoro **lenye kava** kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo 2.5 kwa 6
vi. Mashuka Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*yenye rangi ya pinki)*
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1 jembe 1 **kwa tahasusi za EGM , HGL , PCB na**
xi. Reki 1 na mfagio 1 wa ndani **kwa tahasusi ya HGK na CBG** na Mopa 1 na mfagio 1 wa nje **kwa tahasusi za PCM na HKL**
xii. Scientific calculator kwa wanafunzi watahasusi za PCB, PCM,EGM na CBG Pamoja na mkebe ( mathematical set)
xiii. Aje na begi dogo moja la kusafiria ( mabegi makubwa hayahitajiki kabisa)
xiv. Sanduku dogo imara la kuhifadhia vitu vyake na kufuri (tranka)

xi Mwanaf

## 1.2 Michango mbalimbali ya Shule

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

xix. Kutokuwa / kukosekana bwenini bila ruhusa ( kuwa nje ya shule bila ruhusa)

3. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ..............................................

**Jina la Mkuu wa Shule** David Kindanda ..............................................

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** MKUU WA SHULE SHULE YA SEKONDARI BOGWE S.L.P. 100 KASULU ..............................................

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule:** **0752610950**
- **Makamu Mkuu wa Shule:** **0759013555/0789528064**
- **Mwandamizi Taaluma :** **0623755183/ 0764583787**
- **Mwandamizi Malezi :** **0767886851/0620334517**

## SHULE YA SEKONDARI BOGWE

S.L.P. 100 KASULU

FOMU NAMBA 1

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi.....................................................................................................
2. Jina la baba ............................................................................................................
3. Jina la Mama..............................................................................................................
4. Jina kamili la mlezi........................................................................................................
5. Anuani ya mzazi/mlezi......................................................................................................
6. Uhusiano wa mlezi............................................................................................................
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) ..........................................
8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni...............................................
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni.......................................................
10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni...........................................................................
11. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum.

Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi ...........................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

12. Madhehebu ya dini.............................................................................................................
13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

| | Jina Kamili | Kazi Yake | Namba ya simu |
|---|---|---|---|
| (a) | ...................................... | ............................... | ............................. |
| (b) | ...................................... | ............................... | ............................. |
| (c) | ...................................... | ............................... | ............................. |

Bandika picha

Bandika picha

Bandika picha

**SHULE YA SEKONDARI BOGWE**

**S.L.P. 100 KASULU FOMU NAMBA 2**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Jina la mwanafunzi.........................................................................................................................

Jina la mzazi/mlezi............................................................................................................ Anuani ya mzazi/mlezi................................................................................................... Uhusiano... .................................................................... (mjomba, shangazi, kaka, dada).

Mimi .............................................................................................. nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanfunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania.

Hivyo naahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi.

Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa **BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII** kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi.......................................................tarehe...........................................

Mimi ............................................................................................ mzazi/mlezi wa mwanafunzi ................................................................................ ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi................................................................. Tarehe....................................

**SHULE YA SEKONDARI BOGWE**

**S.L.P. 100 KASULU FORM NUMBER**

**MEDICAL EXAMINATION FORM 03**

To medical Officer I/C of...................................................................................................... Designated Hospital, P.O. BOX ........................................................................................ Please examine the above named in full as to his/her physical and mental fitness for being able to pursue two years of secondary school education. The examination should include categories a-m.

In case of any acute or defect/ disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.

(a) Pupil's name.....................................................................................................

(b) Age .....................................................................................................................

(c) Stool test...........................................................................................................

(d) Blood group......................................................................................................

(e) Urine analysis..................................................................................................

(f) Sphills test .........................................................................................................

(g) Chest test..........................................................................................................

(h) Speech...............................................................................................................

(i) Eye test ..............................................................................................................

(j) Abdomen............................................................................................................

(k) Chest X-ray........................................................................................................

(l) Sickle cell test...................................................................................................

(m)WCB total Differential......................................................................................

Additional information and physical defect or impairment to pursue further studies

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

Signed by ..........................................................................................................

Designation ......................................................................................................

Official Stamp

Date